# AFRI TWENDE

Kulitia moyo kanisa la Afrika katika kazi ya umisheni ulimwenguni

Jarida la 4, Toleo la 1

WWW.AFRIGO.ORG/AFRITWENDE

## WATOTO WA WAMISHENARI: ZAWADI ILIYOFICHWA YA HARAKATI ZA UMISHENI WA KIAFRIKA



Kupitia kwa umakini mabadiliko ya watoto wako

Safari yangu kama mama wa watoto wa wamishenari

Watoto wa Wamishenari wa Afrika Mashariki

# YALIYOMO











## 03 MAONI YA MHARIRI

## 04 KUFUATILIA KWA UMAKINI MAPITO NA MABIDILIKO YA WATOTO WAKO

Uhamaji ni halisi kwa wamishenari. Mojawapo ya ujuzi bora ambao mzazi mmishenari anapaswa kujifunza ni namna ya kuwaongoza watoto watoto katika kukabiliana na mabadiliko.

## 06 SAFARI YANGU KAMA MAMA WA WATOTO WA WAMISHENARI

Mama mmishenari anasimulia safari yake ya kuwatafutia shule sahihi mabinti zake wawili, pamoja na kanuni tano ambazo zitawasaidia wazazi wengine wanaoanza safari kama hiyo.

## 08 WATOTO WA WAMISHENARI WA AFRIKA MASHARIKI

Mkurugenzi wa umisheni anaelezea baadhi ya baraka na changamoto zinazowakabili WWW, Ambazo ni pamoja na lugha, jamii za kimisheni zenye tamaduni mbali mbali na elimu.

## 10 TAFAKARI ZA MTOTO WA MMISHENARI

## 12 MAKUNDI YA WATU: WATOTO WA WAMISHENARI


© 2026 AFRIGO

AFRITWENDE ni chapisho lenye lengo la kuleta ufahamu, uhamasishaji, mafunzo na kusajilisha kanisa na mtu mmoja mmoja katika Afrika kwa nia ya kujihusisha na umisheni duniani.

**Mhariri Mkuu:** Jesse Katabi Masolwa

Ahsante Kwa Furaha Kengela na Emmanuel Lubinza

**Msanifu:** Pilgrim Communications

Maoni yaliyoelezwa katika makala za Gazeti hili siyo lazima yawe ya Mchapishaji.

Picha halisi hutumika inapobidi. Majina hutumika kwa sababu za kiusalama.



Daniel Salamu na familia.

# KUMBATIA

## WATOTO WA WAMISHENARI WA AFRIKA MASHARIKI

Jinsi gani tunaweza kuwakumbatia na kuwalea vyema watoto wa wamishenari wetu katika umisheni? Ni kweli wako katika umisheni, lakini wapo si kwa sababu yao, bali kwasababu ya wazazi wao. Imekuwa ni kawaida kwetu kutoa maelekezo kwao na kutarajia watoto kutii bila kuuliza.

Watoto wangu ni wadogo na walizaliwa baada ya mimi na mke wangu kuwa wamishenari. Hawakuchagua maisha haya, lakini siku moja watachagua. Wanaweza kuikubali au kuikataa kazi hii, kutegemeana na jinsi nitakavyowalea. Ikiwa nitamaliza safari yangu ya umishenari leo, na bado watoto wangu hawaoni jambo lolote jema ndani yake, hilo litakuwa jambo la kukatisha tamaa sana. Badala yake, nataka kuwapa urithi usio na mashaka. Swali la kujiuliza ni: kama wazazi tunawezaje kuishi maisha yenye kuwavutia watoto wetu na kuwapa shauku ya kufuata nyayo zetu?

Nimejifunza kwamba mambo madogo madogo yana umuhimu sana. Sisi watu wazima, tunadhani baadhi ya mambo hayana maana, lakini kwa mtoto yana maana kubwa. Kwa mfano, nilipanga kufanya mkutano muhimu na timu yetu kwenye nchi jirani tarehe 16 ya mwezi. Hata hivyo tarehe 15 ya mwezi huo ilikuwa siku ya kufunga shule kwa mwanangu. Nilisitisha safari na mkutano kwa sababu sikutaka kusafiri siku hiyo muhimu. Nilitaka kuwa pamoja na mwanangu wakati wa hafla au sherehe yoyote na watoto wengine. Uwepo wetu kwenye wakati huo huleta matokeo kwa watoto wetu kwa njia ambayo hatuwezi kujua mpaka baada miaka kadhaa ijayo.

Lazima pia tuwe na nia ya dhati kwa watoto wetu ikiwa tunataka kuona hatimaye umisheni wa kiafrika ukistawi. Ikiwa tutafanya umisheni vibaya, wanaweza kukwambia, “Wewe ndiye uliyechagua kazi hii, sio mimi,” na wanaweza kuacha. Lakini ikiwa wataona kile ambacho wazazi wao wanafanya na kuchagua kumfuata Mungu, basi tutakuwa tukiinua kizazi kipya cha wamishenari na wafadhili wa umisheni. Hata kama hawatakuwa wamishenari moja kwa moja, wataipenda kazi hii na watakua watetezi na wafadhili wa Utume Mkuu.

Tukumbuke jinsi Yesu alivyokwenda Misri wakati fulani alipokuwa mchanga na kipindi cha utoto wake. Baba yake wa mbinguni alimwagiza baba yake wa duniani Kwa njia ya ndoto Yusufu, akimbilie huko. Akiwa na umri wa miaka 12 tunamwona Yesu hekaluni, familia yake ikiwa imerudi Israeli. Labda tunaweza kufikiria jinsi miaka hii ya awali katika ukuaji wake ilivyotumika na utamaduni wa kigeni ulivyoathiri maendeleo ya awali, ufahamu wake wa dunia nzima, na moyo wake kwa watu waliopotea kwa mataifa yote. Ninaamini maisha haya ya umishenari ni maisha bora zaidi ninayoweza kuwapa watoto wangu kwa sababu Mungu aliita familia yangu yote na watoto wakiwa wamejumuishwa. Siku moja nataka watoto wangu waseme, “Baba yangu wa mbinguni na baba yangu wa duniani hawakufanya makosa.”

Katika toleo hili, utasikia kutoka kwa Mkurugenzi wa Ofisi yetu ya Afrika Mashariki, baadhi ya changamoto na Baraka za kuwa mtoto wa mmishenari, utasoma jinsi ya kufanya mabadiliko mazuri kwa watoto kwa kutumia njia ya maridhiano, uhakika na kuangalia mambo yajao, na utasikia habari za mabinti wawili ambao ni watoto wa wamishenari, Baraka na Furaha, ambao hivi leo wanastawi. Maombi yangu ni kwamba utakuja na mtazamo mpana kwa watoto hawa na hata utajitolea kuwaombea na kuombea umisheni kwa ujumla.

---

*Daniel Salamu ni Mkurugenzi wa Ofisi ya SIM iliyoko Afrika Magharibi, ambayo huhamasisha na kutuma wamishenari kutoka mataifa 16. Danieli na mkewe ni wazazi wa WWW watatu: Hadriel, Kirsten-Aurora na Gordon-Bill. Yeye anatoka Nigeria na kwa sasa anaishi Ghana baada ya kutumika kwa zaidi ya miaka 8 nchini Burkina Faso.*

# KUFUATILIA KWA MAKINI

## MAPITO NA MABADILIKO YA WATOTO WAKO

Watoto wa wamishenari ni wahamaji (WWW). Huu ni uhalisia kwa watoto wa familia za kimishenari. WWW huacha nchi zao za asili ambazo kwazo kuna shangazi na wajomba zao, babu, binamu na marafiki na wanafunzi waliosoma pamoja, na kanisa lao lililowatuma. Huanza makazi katika nchi ya kigeni na baada ya muda fulani hutembelea tena nchi zao za asili.

Wakati mwingine wazazi huhamishwa na kupewa eneo na huduma nyingine. Hata kwa WWW ambao wazazi wao hukaa katika eneo moja, wamishenari wengine wanaowazunguka wanaweza kuja na kuondoka, inamaanisha wanapaswa kuwakaribisha na kuwaaga mara kwa mara.

Mojawapo ya mbinu bora ambazo mzazi mmishenari anaweza kujifunza ni namna ya kuwaongoza watoto wao kupita katika mabadiliko, kuwaandaa kusema kwa heri kwa moyo wao wote na kubisha hodi kwa moyo wenye tumaini, na kuwa na utayari wa kuanza ukurasa mpya. Wazazi ambao wana ufahamu na busara wanaweza kusaidia kuendeleza ustahimilivu na ujuzi kwa watoto wao ambao ni pamoja na kuchukuliana na mazingira waliyopo na katika kufanya huduma vizuri kwenye maisha yao yote.




Hebu fikiria juu ya kijito kipana chenye kingo pande zote. Kwenye ukingo mmoja ni mahali ambapo mtoto wako anaishi kwa sasa, na kwenye ukingo wa mbali ni mahali atakapoishi baadaye. Maji yaliyopo katikati ni mapito ambayo yanaweza kupitiwa vibaya, vizuri au katika ustadi mzuri zaidi. Na kwa hivyo pale ambapo dhoruba zisizotarajiwa zikitokea na kufanya njia ya kupita iwe ngumu, kukiwa na mpango wa kuvuka ambao umefikiriwa vizuri utamsaidia mtoto kustawi vizuri hata kama kuna matukio vya kushangaza.

Waandishi wa kitabu kiitwacho 'Third Culture Kids: Growing Up Among Worlds' wanapendekeza hatua nne ambazo kila mtoto wa mmishenari anapaswa kupitia ili kujiandaa kihisia kwa maisha yake mapya. Hatua hizi huwasaidia wazazi kupanga mapito kwa kusudi la kuwaweka watoto wao wawe na muda wa kufikiri juu ya kile

### MASWALI 9 YA KUJIULIZA KABLA YA KUONDOKA

- **Umri:** Watoto wako wana umri gani? Kwa jinsi walivyo wadogo, ndivyo itakavyokuwa rahisi kwao kukabiliana na mazingira. Kwa vijana, mabadiliko yanaweza kuwa magumu sana. Zungumza nao na kupitia uongozi wako ili kuwaandaa.
- **Shule:** Kabla ya kwenda, ni vizuri kujua fursa za elimu zilizopo kwa ajiri ya watoto wako. Unaweza kuhitajika kuleta vitabu vya shule. Gharama lazima zizingatiwe. Uwe na hakika kwamba watoto wako wanaweza kupata elimu wanayohitaji kwa wakati ujao.
- **Lugha:** Je, watalazimika kujifunza lugha mpya katika eneo jipya? Je ni lugha gani mtaizungumza nyumbani kwako? Je, unataka wawe na ufasaha wa lugha mama? utahitaji kuwa na juhudi na kujitolea kwa upande wako ukiwa mzazi.
- **Marafiki:** Je, utaungana na timu ya wamishenari? Kama ndivyo je wana watoto? Je, kuna watoto wazawa wa mahali hapo ambao wanaweza kujenga urafiki nao?
- **Nyumbani:** Ni eneo gani utaenda kuishi? Je, utaishi katika eneo la vijijini, ilihali awali uliishi mjini? Je itakuwaje kwa watoto wako tokana na tofauti hiyo?
- **Huduma za matibabu:** Je, unajua namna utakavyopata huduma za afya kwa watoto wako ndani ya makazi mapya? Je, watoto wako wana mahitaji yoyote maalum ya kiafya? Ni kwa namna gani utalipia gharama za afya?
- **Dharula:** Je, misheni yako au ubalozi wa nchi yako utakusaidia iwapo kutakuwa na mgogoro wa kisiasa au janga la asili katika eneo lako jipya la huduma?
- **Kiwango cha maisha:** Ni hali gani ungependa zaidi uweze kuwa nazo kwenye mazingira mpya, iwe juu au chini kuliko vile ambavyo watoto wako wamezoea? Utawaandaaje watoto wako kwa viwango tofauti ya maisha?

kinachokuja, huku wakiwa na uhakika wa kuagana vizuri na kuondoka kwa moyo mkunjufu na kwa njia bora. **Hatua hizo nne ni upatanisho, uthibitisho, kuaga na kufikiri juu ya hatima.**

## Upatanisho

Upatanisho unahusu kuweka mambo sawa katika mahusiano ambayo yataachwa nyuma. Inamaanisha kukaa chini na kusuluhuhisha magonvi au migogoro yoyote na watu wengine. Kuomba au kutoa msamaha huondoa wasiwasi kwenye moyo wa mtoto na humuaandaa kuenenda katika mahusiano mapya kwenye makazi yajayo. Njia mbadala ambayo ni yenye majaribu ni kuyahifadhi matatizo ya eneo moja na kuyaacha nyuma. Hii haiwezi kukusaidia kwenye huduma; kwa sababu kila mmoja wetu anajipeleka mwenyewe na mazoea yake pamoja nasi katika maeneo mapya. Upatanisho ni jambo ambalo mtoto anaweza kulitumia katika maisha yake yote.

## Uthibitisho

Uthibitisho unamaanisha hali ya kuonyesha thamani ya mahusiano muhimu ambayo yataachwa nyuma. Ni watu gani na kumbukumbu zipi zinaweza kuthibitishwa na kuthaminiwa? Je, ni nani ambaye wewe na watoto wako mnaweza kumshukuru kwa ushawishi na mchango wake kwenye familia yako? Hakikisha mnapiga picha pamoja, unaandika jumbe za shukrani, au kutoa zawadi maalumu ili kukumbukana. Hatua hii itamsaidia mtoto wako kukumbuka nyakati nzuri na watu wazuri kwa wakati mrefu ujao. Mchakato huu utamruhusu mtoto wako kupitia mabadiliko chanya.

Kulikuwa na mafunzo kwa wamishenari wapya waliofika kutumika nchini Burkina Faso. Watoto katika familia moja walikuwa wameambiwa na wazazi wao kwamba wanaweza kuchagua kitu kimoja au viwili maalumu kutoka nchini kwao ili kuvileta nchi mpya waliyohamia. Wazazi waliwaahidi kufungasha vitu hivi na kwenda navyo Burkina Faso. Je unajua mtoto mmoja alichagua nini? Aliokota mawe madogo madogo kutoka nchini kwake! Kwa hiyo kokoto hizi muhimu zilifungwa na kufika na mizigo huko Ouagadougou, kama ilivyoahidiwa.

## Kwa Heri

Kwa heri ni kitendo cha kuagana. Inaweza kuonekana ni jambo la kawaida sana kulitaja, lakini katika harakati za kuwahi kuondoka, hupunguza nafasi ya watu kuagana vizuri na jambo hili huachwa mpaka dakika ya mwisho kabisa. Unapoharakisha kuaga huacha mambo mengi bila kusemwa na inaweza pelekea kuhisi kutoridhisha. Kuagana sio tu kwa watu maalum, lakini pia hata kwa maeneo kama vile shule yao au mgahawa pendwa, matukio au mila ambazo walizijua mara kwa mara, na hata kuaga vitu. Andaa orodha ya watu, maeneo uliyotembelea mara ya mwisho na ambayo yalikupa uzoefu na lipe nafasi jambo hili wiki chache kabla hujaondoka. Andaa sherehe ya kuwaaga marafiki wa mtoto wako. Mkiwa wazazi ambao hutingwa na majukumu mengi huku mkipanga hatua zijazo wanapanga kwa bidii hatua zinazofuata, kupakia mizigo, na kukamilisha kazi za huduma, hakikisha unachukua muda wa kuaga, panga tarehe kwenye kalenda. Kusema kwaheri kunaumiza lakini ni muhimu kufanya hivyo kabla ya kuchukua hatua nzuri kuelekea eneo linalofuata.

## Fikiria juu ya ukomo wa Safari

Fikiria mahali unakoenda ina maanisha kujifunza na kuota ndoto juu ya eneo jipya. Hebu waza pamoja na watoto wako ni kwa namna gani itakavyokua mkifika huko. Fanya utafiti kwenye mtandao. Andika sifa nzuri za kuhamia eneo jipya na manufaa yatakayopatikana pamoja na mambo mtakayopata huko. Msaidie mtoto wako ajione kwenye mazingira mapya – katika shule mpya, nyumba mpya; chukua hatua kwa matendo kujiandaa kwa ajili yake. Ni sawa kujihisi kuwa na shauku juu ya eneo jipya na itakuwa ni vigumu kama unahisi huzuni kuliaga eneo unalolifahamu na ulilokua unalipenda. Ni muhimu kumwambia mtoto hivi kuwa ni lazima, ni sawa hata kwa wao kuwa na huzuni, haswa wakati kama huu kuna hisia tofauti tofauti huinuka juu ya jambo jipya linalokuja.

*Imechukuliwa kwenye kitabu cha Third Culture Kids; Growing Up Among Worlds na Dave Pollock na Ruth Van Reken.*

- **Familia:** Je, watoto wako wana uhusiano gani wa karibu na binamu, shangazi na wajomba au babu na bibi? Je una mpango gani wa kudumisha uhusiano huu kutokea mbali? Je unaweza kupiga simu za intaneti mara kwa mara.
- **Vitu vyenye thamani:** Je! mtoto wako ana vitu vya thamani kama vile wanasesere, michezo, au nguo ambazo wanataka kwenda nazo? Ni vizuri kuzungumza nao kuhusu mapungufu na kuwapa uhuru wa kuchagua, ili waweze kuona kuwa nao ni wahusika katika maamuzi ya wa jambo hili jipya kwa ajili ya familia.



# SAFARI YANGU KAMA MAMA WA WWW

*Majina ya watu na mahali yamebadilishwa kwa ajili ya usiri



Mimi na mume wangu tuna wasichana wawili, Blessing na Joy. Wakati tulipokuwa tukijiandaa kuitikia wito wa Mungu wa umisheni wenye mchanganyiko wa tamaduni nchini Thailand, shirika letu lilituarifu kwamba eneo tulilopewa lilikuwa na mwalimu wa shule ya nyumbani kwa ajili ya watoto wa familia mbili, tayari alikuwa anahudumu huko. Tulitiwa moyo kwamba Baraka, aliyekuwa na umri wa miaka minane wakati huo, angeanda pamoja nasi kwenda shambani mwa BWANA na kujiunga na kikundi hiki cha shule ya nyumbani. Baada ya kutafuta ushauri na maombi, tuliamua kwamba binti yetu mkubwa, Furaha, atakaa na ndugu katika nchi yetu ili kuanza masomo ya ngazi ya chuo kikuu. Ingawa kulikuwa na elimu ya chuo kikuu nchini Thailand, ilikuwa katika lugha ya wazawa.

Tuliwasili tukiwa tumejaa nguvu na muda mfupi badae tulipata makazi nje ya mji. Ndani ya majuma kadhaa ya tangu tulipowasili, mwalimu wa shule ya nyumbani aliondoka. Hakukuwa na walimu wengine mahali pale.

Familia hizo mbili hivi baada ya muda mfupi ziliamua kuhamia tena kwenye mji mkuu ambapo kulikuwa na elimu yenye kiwango bora zaidi. Mimi na mume wangu, kwa haraka tukitimiza majukumu ya uongozi kwenye eneo letu la huduma, tuliendelea na maombi kwa kila machaguo yote ya kielimu ambayo tuliyafikiri. Hatimaye familia nyingine ya wamishenari toka Afrika Magharibi iliwasil kwenye mji mwingine ulio umbali wa masaa manne kutoka kwetu. Tulipanga kuwa binti yetu, Blessing aende akaishi nao na kuhudhuria shule ya nyumbani kwenye mji huo, kwa bei nafuu na ni karibu kuliko mji mkuu.

Ninaweza kukwambia kwamba tulipomtafuta BWANA kwa bidii katika maombi, mambo haya mawili hayakua rahisi kuafikiana nayo kwa ajili ya binti zetu, Neema ya Mungu imekuwa kubwa kwetu, na ninaweza shuhudia kwamba wasichana wote wawili wanaendelea vizuri hivi leo.

Neema ya Mungu imekuwa kubwa kwetu, na ninaweza shuhudia kwamba wasichana wote wawili wanaendelea.

www.afrigo.org/afritwende

Hata hivyo, haikuwa safari iliyokosa changamoto.

Binti yetu mkubwa, Joy, alihisi kwamba kazi yetu ya umisheni ilikuwa "imetuiba" sisi kutoka kwake. Kuishi na ndugu yetu kulikuwa na shida sana kiasi kwamba ilimlazimu mume wangu kurudi nyumbani kusaidia kuitatua. Kipindi cha maisha ya ujana, wanapotoka nyumbani na kufikia hatua za awali za utu uzima kimejawa na vikwazo, hata kama ni kwenye mazingira mazuri. Miaka miwili baadaye wakati wa mgogoro nchini kwetu, shirika letu la umisheni ilifanya bidii kumtunza na kumlinda binti yetu. Kupitia mwitikio wa misheni katika kipindi hiki cha hatari, Joy alipata upendo wao mkubwa. Leo tunamsifu Mungu kwamba Joy ni msichana aliyefanikiwa.

Na pia mpango wa Blessing ulikuwa mzuri kabisa, japo haukukosa changamoto. Tulimpa simu ili atupigie mara nyingi kadiri ilivyohitajika. Familia wenyeji walikuwa na ukarimu wa kweli na makini kwa mahitaji yake yote. Lakini familia ambayo si yako inawezaje kumwadhibu mtoto wa mtu mwingine pale ambapo hafanyi kazi za shule? Matokeo yake kitaaluma yaliathirika kwa namna fulani. Adha au aibu ni jambo lisiloepukika kwa mtoto anayeishi na familia nyingine. Hata alipopokelewa kwa uchangamfu hatukuweza kumsaidia Baraka kutoka kwenye mawazo ya kuhisi pengine labda wazazi wangu hawanitaki, hisia ambazo si za ukweli!!

Kama wazazi, hasa wazazi wa WWW, tunajifunza kila wakati. Acha nitoe baadhi ya kanuni tulizokusanya njiani:


1. Washirikishe watoto wako kwenye majadiliano kuhusu mabadiliko yajayo, nini kitatokea, jinsi kitakavyotokea. Hata vijana wadogo wana hisia, mawazo na maoni. Waache waongee.
2. Wasaidie watoto wako kupitia mabadiliko. Sio tu mtazamo wako mzuri, lakini pia waruhusu kuchukua kitu ambacho ni maalum au chenye kuwafariji, wape uhakika wa usalama popote watapokuwa.
3. Panga mipango, tena na tena... na uwe tayari kwa mambo ya kushangaza. Licha ya mipango bora, timu za umisheni na rasilimali za misheni zinaweza kubadilika mwaka hadi mwaka. Machaguo yako ya mwaka mmoja huenda yasiwe sawa na ya mwaka ujao.

## Usiwe mwenye hofu kuukwepa wito wa Mungu wa umisheni. Malezi yana changamoto hata kama unakaa nyumbani.

4. Wakala wa umisheni na kanisa linalotuma lazima wajue vizuri juu ya shule za mahali watakapokwenda wamishenari. Haijalishi kazi fulani ni ya dharura au ya kimkakati kiasi gani, mahitaji ya watoto ni muhimu vile vile.

### CHANGAMOTO ZA KIPEKEE KWA WAAFRIKA

- Ndani ya Afrika, WWW wa Kiafrika mara nyingi "hufichwa" kwa sababu huwa wanachanganya. Wamishenari wengine na watu wa eneo hilo wanaweza wasifikirie kuwa wao ni WWW kwa sababu hawajazoea kuwaona Waafrika katika kazi na majukumu kama haya.
- WWW wanaweza kuwa na changamoto kubwa za lugha kwa kuhitaji kujifunza lugha mama na lugha ya biashara ya wazazi wao, lugha ya wazawa pamoja na lugha ya biashara ya mahali ambapo wazazi wao wanahudumu, pamoja na lugha ya kujifunza shuleni! Familia ya wazawa inaweza isijue jinsi ya kuwakubali kikamilifu WWW wako ambao wamekuwa tofauti na binamu zao au marafiki wa nyumbani. Maneno yenye kumdhihaki mtoto wako kwa rejareja kwa kutozungumza lugha ya wazazi wake vizuri, kutokula kama wao, na kuelezea tofauti zingine. Hata kwa mzaha, maneno haya yanaweza kufikisha ujumbe hasi au wa hila kwa WWW kuhusu utofauti wao.



5. Kuishi katika tamaduni mbalimbali kutawatengeneza, kutawastawisha na kuwachanganya wanao. Wasaidie kuelewa tofauti za tamaduni na kuwasaidia kujibu kwa ujasiri maoni toka kwenye familia yako, watu wa eneo lako, na wamishenari wa mataifa mengine. Mstari kwa ajili ya watoto wangu ulikuwa 1 Petro 3:15, "Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu;lakini kwa upole na kwa hofu".

Usiwe mwenye hofu kuukwepa wito wa Mungu wa umisheni. Malezi yana changamoto hata kama unakaa nyumbani. Kufuata mapenzi ya Mungu kwako na familia yako daima ni mahali na jambo sahihi kutenda. Mojawapo ya mistari ninayopenda ni Isaya 30:21 "na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni; mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto." Hii ndiyo njia; tembea katika njia hiyo.

Ikiwa tunatafuta hekima ya Mungu, panga vizuri, na kujitoa kwa watoto wetu wakati wa changamoto, basi tuna kila tumaini watakua watu wenye uelewa mzuri na ufahamu mzuri. Na Mungu atawaongoza katika majukumu ambayo malezi yao ya kipekee baadae hata yakiwa na changamoto utakuwa umewaandaa kitamaduni. Kama mwandishi mmoja alivyosema, "matuta ni yale wanayopanda juu yake." Kwa msaada wako, watoto wako na wapande juu kwa ajili ya Mungu.



# WATOTO WA WAMISHENARI WA AFRIKA MASHARIKI

NA WORKU HAILEMARIAM

Wongel Mulugeta Wongel (Injili) Zeleke, William Cary, Ephrem Getachew - haya ni majina ya baadhi ya watoto wa wamishenari wetu (WWW) ambao wanawakilisha ujumbe wa injili na maisha ya wamishenari. Kupitia majina ya watoto wao, wamishenari wetu hukumbushwa juu ya wito wao.

Kuandaa familia na watoto wao kwa ajili ya maeneo mapya huwa na changamoto. Ni muhimu kwa kanisa linalokutuma na misheni kufanya kazi pamoja kwa karibu kwenye maandalizi, ikiwa ni pamoja na matarajio juu ya changamoto zitakazokuja na jinsi ya kuzishughulikia kwa pamoja. Kwa njia hii, baadhi ya matatizo yanaweza kupungua. Kama ilivyo, familia za wamishenari na WWW ambazo tunakabiriwa na changamoto kwa pande zote mbili katika kipindi cha kutumwa na kupokelewa - changamoto ambazo ni za kihisia, kifedha, na kijamii.

## Lugha

WWW wa Kiafrika kwa kawaida wanatarajiwa kuzungumza angalau lugha tatu. WWW kutoka katika muktadha wetu wa Kiethiopia huzungumza Kiamhariki, lugha yetu ya kitaifa. Aidha, wanajifunza lugha ya asili ya wazazi wao; lugha ya kimataifa kama vile Kiingereza, Kifaransa, au Kiarabu; na hatimaye, lugha ya kitaifa ya nchi ya utumishi, kama vile Kiurdu au Kichina. Katika hali nyingine, lugha ya asili kutoka nchi ya huduma pia huongezwa. Mara nyingi wazazi hupendelea kutumia lugha zao ya asili za kikabila baina yao lakini hutumia Kiingereza au lugha ya huduma ya eneo husika kwa watoto wao. Hata hivyo, kuna wengine wanapendelea kuwafundisha watoto wao lugha ya asili ya wazazi wao.

> Wakati familia zinapotengana, watoto wanaweza kuhisi kutelekezwa, na hata kuwa na uchungu kwa BWANA kwa kuchukua wazazi wao. Mzazi anaweza kufanya nini?

Kwa upande mmoja, watoto walio katika mazingira ya kuzungumza lugha tatu au zaidi wakati wa miaka yao ya awali watapata lugha za ziada kwa urahisi zaidi. Kwa upande mwingine, kwa muda mfupi, uwepo wa lugha nyingi unaweza sababisha watoto kuchelewa kupata elimu kwa sababu ujuzi wa lugha ya elimu inayotakiwa unakua bado haujakamilika.

## Changamoto za Kiutamaduni

Kila mmishenari anatarajia kuishi katika utamaduni wa kigeni, lakini utamaduni mchanganyiko wa jamii ya wamishenari wa mataifa mengi unaweza kuwa wenye kushangaza. Baadhi ya maeneo, watoto hujiunga na jamii mbalimbali bila ufahamu wa makundi madogo au makubwa ya tamaduni. Hata hivyo, katika maeneo mengi WWW wa Kiafrika ni kundi la wachache kikabila na kitamaduni. Katika kutilia mkazo hili kunaweza pelekea upweke na kujitenga, kama ambavyo WWW walivyosema wakati familia yao iliporudi kwenye nchi yao kwa 'majukumu ya nyumbani, "Tungetamani kubakia kwenye nchi yetu ili kuweza kuwa na marafiki wengi."

## Elimu

Ukosefu wa fedha daima ni suala lenye changamoto kubwa sana pia kwenye elimu ya watoto. Matarajio ya kawaida ya kanisa linalotuma na jamaa ya wamishenari ni kwamba WWW wataweza kupata elimu bora zaidi nje ya nchi yao. Wanadhani popote pale misheni itakapokua inahudumia,

www.afrigo.org/afritwende

shule nzuri zitakuwepo. Hata hivyo, huu sio uhalisia kila wakati. Dhana ya pili kutoka kwa kanisa linalotuma ni kwamba gharama ya elimu ya watoto inaweza patiwa ufumbuzi. Hata hivyo, huu pia sio uhalisia.

Kwa upande mmoja, wamishenari wanahangaika kulipia elimu ya watoto wao; kwa upande mwingine, makanisa yanahangaika haswa kuongeza zaidi msaada wa kifedha. Matokeo yake, wazazi wamishenari hubeba mzigo wa ziada wa kutafuta njia za kuongeza ufadhili kwa watoto wao, jitihada hizi zinaweza kusababisha wasiwasi na msongo wa mawazo.

Wamishenari wa Kiafrika hawajui juu ya shule za nyumbani na masomo ya nyumbani na pia hazitambuliwi katika nchi zao.

## Kutelekezwa

Mara nyingi, watoto wa wamishenari lazima kupelekwa shule, mara tu wanapokuwa wakubwa. Hii inaweza kuwa kwa sababu hakuna shule nzuri kwenye eneo husika, au wazazi hupendelea watoto wasome shule kwa lugha yao wenyewe. Au, masharti yanaweza kuwa magumu kwenye eneo ambalo wazazi wanatumika na wazazi huhisi watoto watakuwa huru zaidi mahali pengine. Wakati mwingine watoto huachwa kwenye nchi za nyumbani, pamoja na ndugu, kwa ajili ya shule.

Wakati familia zinapotengana, watoto wanaweza kuhisi kutelekezwa, na hata kuwa na uchungu kwa BWANA kwa kuchukua wazazi wao. Mzazi anaweza kufanya nini? Ni muhimu kwa wazazi kuwasiliana kwa uwazi na watoto wao kuhusu fursa na zipi zitakua bora kwa muda mrefu. Uhusiano wenye na wa kusaidiana, unaweza kuwasaidia watoto kuhisi hawapelekwi mbali au kuachwa nyuma.

Mara baada ya mtoto kutenganishwa na mzazi, mawasiliano ya mara kwa mara ni muhimu na mtoto lazima ajisikie huru kuwashirikisha wazazi jambo lolote linalomtatiza. Ingawa ni rahisi kutingwa sana na huduma, kumbuka kwamba wewe kwanza ni mzazi na kazi ya pili ni mmishenari.

Licha ya gharama kubwa ya kufanya kazi ya umisheni haswa kwa elimu ya watoto, ninaweza kushuhudia kwamba baadhi ya makanisa ya Kiafrika yanawasaidia wamishenari wao kwa kujitolea sana. Hawatoi msaada kulingana na "unafuu" ilivyo kwao. Badala yake, kama Paulo anavyosema katika 2 Wakorintho 8:3: "Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao."

Nimeona kwamba baadhi ya makanisa yanayounga mkono huduma, japo majengo yao wenyewe kanisa yako katika hali duni na kuna vipaumbele vingine, yamejitolea kutoa kipaumbele cha kwanza kwa msaada wa mmishenari.

Haya yote yamesemwa, kwa kuwa tumefanya ziara za kimishenari kwa watu waliotumwa kutoka Ofisi yetu ya Afrika Mashariki, tumeona uwezo wa kushangaza na ustahimilivu wa WWW wetu. Wengine wanaweza kuwa marubani wamishenari, wahudumu wa tamaduni mchanganyiko, na walimu wa WWW wengine. Hili linatia moyo na tunaona kuwa tunaweza kuzalisha kizazi cha pili cha wamishenari.



*Worku Hailemariam ni Mkurugenzi wa Ofisi ya SIM ya Afrika Mashariki huko Addis Ababa, Ethiopia, akihudumu kutoka 2012 hadi 2023. Ofisi hii inahamasisha, inaelekeza, na kuwatuma wamishenari kutoka Afrika Mashariki kuhudumu ulimwenguni kote. Makanisa ya Ethiopia yamekuwa yakituma wamishenari tangu miaka ya 1990.*



Picha na Freepik

# TAFAKARI ZA MTOTO WA MMISIONARI

## na Eliya Shilikale




Watoto wa wamishenari hukua katika maisha yenye imani, kujitoa, na kusudi maalum. Utoto wao huwa tofauti kwa sababu hukulia katika maeneo ambako wazazi wao wanahudumu wakihubiri Injili, kupanda makanisa, kutafsiri Biblia, na kuishi karibu na jamii zinazowazunguka. Maisha yao yanaonyesha wazi kuwa kazi ya Mungu si ya mtu mmoja tu, bali ni ya familia nzima.

Tangu wakiwa wadogo, watoto wa wamishenari huona huduma ikifanyika kila siku. Wanawaona wazazi wao wakiomba, wakimtegemea Mungu, na kuvumilia changamoto. Kwa sababu hiyo, imani yao hukua katika maisha halisi, si katika mafundisho pekee. Huduma kwao si kitu cha kusikia tu, bali ni kitu wanachoishi.

Watoto wengi wa wamishenari hukua wakihama kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kukutana na tamaduni tofauti. Wengine hukua miongoni mwa makabila kama Wamaasai, wakijifunza maisha rahisi na ya kijamii. Wengine hukaa katika jamii zilizoathiriwa na dini nyingine, wakijifunza kuheshimu watu huku wakimshuhudia Kristo kwa upole. Pia wapo wanaoona kazi ya tafsiri ya Biblia ikifanyika miongoni mwa makabila kama Wahadzabe, ambapo kusikia Neno la Mungu kwa lugha yao huleta uelewa na mabadiliko ya kweli. Uzoefu huu humsaidia mtoto wa mmishenari kuelewa tamaduni, kuona uhitaji wa kiroho, na kushuhudia nguvu ya Injili.

Kukua katika huduma kunajenga pia imani yao binafsi. Watoto hawa hushiriki mapema katika huduma kama kusaidia watoto, kushiriki ibada, au kusaidia miradi ya jamii. Wanajifunza kumtegemea Mungu wakati wa magonjwa, changamoto za kifedha, au mazingira magumu ya kiroho.

Hata hivyo, watoto wa wamishenari hukutana na changamoto kama kuaga marafiki mara kwa mara, kujifunza lugha mpya, au kuhisi hawana mahali pa kudumu. Changamoto hizi huwajenga kuwa wavumilivu, wakomavu, na wenye huruma.

Kwa msaada wa familia, makanisa, na mashirika ya misheni, watoto wa wamisionari hustawi. Wengi hukua wakiwa na upendo kwa Neno la Mungu na moyo wa kuwahudumia watu. Maisha yao yanatukumbusha kuwa misheni ni kazi ya familia nzima, na Mungu hutumia hata watoto kuendeleza kazi Yake duniani. Tazama nakala ndefu zaidi https://bit.ly/EShilikale

---


*Eliya Shilikale ni mtoto wa mmishenari kutoka Tanzania na mwanafunzi katika shule ya Simba wa Yuda anayesoma pia tafsiri ya Biblia katika Chuo Kikuu cha Dallas International University na ana moyo wa kuona watu ambao hawajafikiwa wakipokea Neno la Mungu.*

---

## Fahamu zaidi kuhusu AfriTWENDE!

Kwenye tovuti yetu, tuna matoleo matano ya Kiswahili! Kila toleo lina makala ambayo itakufundisha zaidi kuhusu umisheni, kukuarifu kuhusu kile wamisionari wanafanya shambani, na kukuchochea kuwa hodari katika imani yako. Unaweza kuona makala yote na kupakua masuala bila malipo kwenye tovuti yetu kwa www.afrigo.org/afritwende.






## Pata nyenzo za bure za kukusaidia kuelewa Uislamu na kufikia jirani yako

Ndugu na dada, msisahau kwamba unaweza kufikia rasilimali nyingi za bure na za gharama nafuu kwenye Uislamu kwenye tovuti ya AfriTWENDE. Hizi zimetolewa na LifeChallenge Afrika, na unaweza kusoma na kupakua baadhi bila malipo kwenye tovuti yetu. Au, unaweza kufuatilia kwenye tovuti yao ili kuona karatasi na vitabu zaidi kwa gharama nafuu. Lengo lao ni umhubiri Yesu kwa na Waislamu na huduma yao imefanya kazi ya kutengeneza rasilimali katika lugha za Kiingereza, Kiswahili, Borana na Kisomali. Je, una wanafamilia au majirani wanaofuata Uislamu? Nyenzo hizi zitakusaidia kujua jinsi ya kuzungumza nao kuhusu Yesu, au kukusaidia kuelewa zaidi yale ambayo. Uislamu unafundisha ukilinganisha na Biblia. Tembelea https://bit.ly/4q7EsAD.

## "Kujawa wasiwasi, malalamiko na shaka"

Katika mwaka wa pili wa maisha yetu kwenye kazi ya umisheni, changamoto ya kifedha na kupungukiwa kila mara lilikuwa ni jambo moja ambalo lilitufanya kuhoji wito wetu kwa Mungu.

Nakumbuka wakati mmoja ulikuwa mgumu sana. Kulikuwa na mahitaji ambayo hayajatimizwa na mengi zaidi yalitarajiwa. Wakati huo mimi na mke wangu tuliamua kwenda sehemu tulivu, ya upweke ili tuzungumze na labda kuomba.

Tuliacha simu zetu nyumbani ili kuepuka usumbufu.

Wakati wetu pamoja ulikuwa umejaa wasiwasi, malalamiko na mashaka ikiwa kweli Mungu ndiye ambaye alituita kwenye kazi ya umisheni.

Tulirudi tukiwa tumekata tamaa. Lakini nilipoangalia simu yangu, nikakuta mtu ametutumia pesa. Kwa hakika nilijua wakati huo huo kwamba ni Mungu anayejibu malalamiko na mashaka yetu. Kisha tukatambua kwamba Mungu alikuwa amejitolea kutupatia mahitaji yetu ya kila siku tunapomtumikia. Mara nyingi tunataka kesho yetu iwe na uhakika wa mahitaji, lakini Mungu kwa uaminifu hutupatia mahitaji yetu ya kila siku. Tunaendelea kumwamini kwa neema ya kumtazama kama usalama wetu hata tunapomtumikia.

Bado tunapitia changamoto lakini kwa tumaini na imani kwake yeye aliyetuita na anataka kututumia kwa utukufu wake kati ya watu ambao bado hawajamjua.

\- Wanandoa wamishenari kutoka Uganda wakiwafikia watu wa Karamajong.




## Tufuate kwenye media

Tupate kwenye Facebook kwa www.facebook.com/AfriTwende au kwenye Instagram kwa www.instagram.com/afritwende/ Kuona hadithi mpya za wamisionari kila juma, kusoma makala za kuvutia, na kutiwa moyo. Unaweza pia kwenda kwenye ukurasa wetu wa hadithi za wamishonari wa Kiafrika ili kusoma hadithi zote za wamisionari ambazo tumetengeneza.




# Makundi ya Watu: WWW

Watoto wa Wamishenari, wanaojulikana kama WWW, wamekuwa sehemu ya historia ya umisheni tangu zama za Umisheni wa Kisasa ulipoanza mwishoni mwa miaka ya 1700. Lakini hadi miongo ya hivi karibuni, sifa zao za kipekee na majukumu yao ya kipekee ya kimisheni yameeleweka kidogo tu na kwa sehemu kubwa hayajarekodiwa. Leo michango yao, uzoefu wao wa kipekee wa maisha na sifa zao zenye kufaa zinajulikana na kueleweka vizuri zaidi.

Uzoefu wa WWW juu ya tamaduni na watu wengine imewawezesha kuishi kipekee na kuwandaa kukabiliana na ulimwengu wa utu uzima. WWW wengi huwa viongozi makanisani, na katika huduma zingine ulimwenguni. Henry Luce alizaliwa na wazazi wamishenari nchini China mnamo 1898. Alipokuwa mtu mzima alianzisha gazeti la Time la kwanza na la aina yake na bado ni gazeti la habari linalosambazwa kila juma mpaka sasa ni moja ya gazeti linalosambazwa kwa wingi duniani. Mitazamo aliyopata kipindi cha utoto wake ilichochea maono yake katika uchapaji wa habari za kimataifa.

Neno jipya, Watoto wa kizazi kipya, liliundwa katika miaka ya 1950 na mtafiti Ruth Useem. "Mtoto wa kizazi kipya ni mtoto ambaye, sehemu kubwa ya maisha yake na makuzi na maendeleo yapo katika utamaduni tofauti na wa nyumbani kwa wazazi wake na huendeleza mahusiano na tamaduni zote, japo akiwa hana umiliki kamili katika tamaduni yoyote ile kati ya zote alizokulia. Mambo mbali mbali wanayoyaishi na kuyazoea kutoka kwenye kila tamaduni hujumuishwa kwa kadri anavyozidi kukabiliana na jamii hiyo, na hisia ya kujisikia kuwa ni mtu wa sehemu fulani husika huwa sawa na watoto wengine wanaoishi kama yeye." Watoto wa kizazi kipya ni pamoja na WWW, watoto wa wafanyabiashara, wanadiplomasia, na wafanyakazi wengine wa kimataifa.

Watu wazima ambao ni WWW wengi hushikilia malezi yao, baraka na changamoto zao, na uzoefu wa kipekee ambao umewatengeneza. Lakini kama watoto wote wa wazazi wa Kikristo, wanaweza vile vile kuchagua kuachana na imani.

## Kwa Kuangalia/Kwa Ufupi

- WWW hupata uzoefu na ujuzi wa kufanya kazi vizuri ndani ya tamaduni mbalimbali.
- WWW wanaweza kujisikia wametelekezwa na watu/wazazi mahali au kwenye nyumba tofauti tofauti na kukosa mahali/nyumba moja sahihi watakapopaita nyumbani.
- WWW wanatatizika kujua ni wapi wanastahili.

## Mwombe Mungu:

- Kutoa mpango mzuri wa utume na viongozi wa kanisa jinsi ya kusaidia familia nzima kuingia katika wito wa Agizo Kuu.
- Kuwasaidia WWW wakati wa mabadiliko ya kuhama kutoka nchi yao hadi kwenye nchi na makazi mapya ya huduma na shule.
- Awarudishe kwake WWW ambao hawamfuati Mungu.

*Tafsiri kutoka Third Culture Kids: Growing up Among Worlds na David Pollock na Ruth Van Reken

AFRITWENDE: afritwende@afrigo.org AFRIGO: info@afrigo.org ALLONS-Y ! : info@afrigo.org AFRÍDE: afride@afrigo.org

**SIM Afrika Mashariki**
Sm: +251 911 206 530
east-africa.office@sim.org

**SIM Afrika Magharibi**
Sm: +233 30 222 5225
wamo.personnel@sim.org

**SIM Kusini mwa Afrika**
Sm: +27 21 7153200
southafrica.mobilisation@sim.org

**AIM Kimataifa**
amc.io@aimint.org
aimint.org/africanmobilization/